


# SHERIA YA AJIRA NA MAHUSIANO KAZINI, NO. 6, 2004

***EMPLOYMENT AND LABOUR RELATION ACT, 2004***



# EMPLOYMENT STANDARDS

## (VIWANGO VYA AJIRA)

***(Kifungu cha 12 – 44 SAMK)***


**Martha A Lwitiko**

**Tanzania Labour College**

**0763 006 000**

# Maana ya Viwango Vya Ajira



- Ni Masharti ya msingi ktk ajira ambayo kila mwajiri anapaswa kuzingatia
- Ni Vipimo vya ubora vilivyowekwa na mamlaka ya kazi ili kurekebisha mazingira ya kufanyia kazi

# DHUMUNI LA VIWANGO VYA AJIRA



- Kuwalinda wafanyakazi wasiingie ktk mikataba ya ajira isiyo ya haki
- Kuwaepusha wafanyakazi wasiweze kutumiwa na Mwajiri nje ya viwango vilivyowekwa

## SAA ZA KAZI



## TARATIBU ZA MALIPO



# VIWANGO VYA AJIRA

## LIKIZO *(Leave)*



**SAA ZA KAZI (Hours at work)**




**ILO Convention No. 1, 1919:**

- ✓8hrs at work
- ✓8hrs at home
- ✓8hrs sleeping

# Normal Working Hours
# (Saa za Kazi za kawaida)
***(Kifungu No. 19 SAMK)***



**SAA 45 KWA JUMA/WIKI**

**SAA 9 KWA SIKU**

**NB:**
**SHERIA INAZUIA MFANYAKAZI KUFANYA KAZI ZAIDI YA SAA 12 KWA SIKU YOYOTE ILE**

# SIKU ZA KAZI (working days)

*(Kifungu No. 19 SAMK)*

- SIKU ZA KAZI NI 6
- IWAPO MFANYAKAZI ATAFANYA KAZI SAA 9 KWA SIKU ATAFANYA KAZI SIKU 5 KWA WIKI
- NA YULE ANAYEFANYA KAZI SAA 8 KWA SIKU ATAFANYA KAZI SIKU 6 KWA WIKI

**NB:**

**MFANYAKAZI ANAYEFANYA KAZI SAA 9 KWA SIKU ANAWEZA KUFANYA KAZI SIKU YA SITA AMBAYO ITAHESABIWA KAMA SAA ZA ZIADA**



# SAA ZA ZIADA (OVERTIME)

*(Kifungu No. 19 SAMK)*

KAZI ZA ZIADA ZIFANYWE KWA MAKUBALIANO

SAA ZA ZIADA ZISIZIDI 3 @SIKU NA SAA 50 @MWEZI

MALIPO YA SAA ZA ZIADA NI MARA MOJA NA NUSU (1.5) YA MSHAHARA WA SAA KWA KILA SAA LA ZIADA



# MFANO

***Mshahara wa Janet ni Tsh.300,000/= kwa mwezi. Janet amefanya saa za ziada 30 kwa mwz, je Janet atapata sh. Ngapi kwa mwz huo?***

**Tafuta mshahara Wa saa**

$$\frac{300{,}000}{4.33 * 40} = 173$$

$$\frac{300{,}000}{173} = 1{,}734.10$$

**Saa za ziada**

**1,734.10*1.5*30**

**= *78,034.5***

**Mshahara wa mwezi**

**300,000+ 78,034.5**

**= *378,034.5***



# KAZI ZA SIKU ZA SIKUKUU

*(Kifungu No. 25 SAMK)*

**Mshahara wa kazi wa siku za sikukuu Ni mara 2 ya Mshahara wa Saa kwa kila saa**

# KAZI ZA USIKU
## *(Night work)*
***(Kifungu No. 20 SAMK)***

**Kazi zote zinazofanywa Kati ya saa 2.00 usiku na Saa 12.00 alfajiri.**

**Mwajiri haruhusiwi kuwapa kazi za Usiku wafanyakazi wafuatao:**

- ☑ ***Wajawazito waliobakiza miezi 2 kabla ya tarehe ya kujifungua au zaidi kwa ushauri wa daktari***
- ☑ ***Wazazi miezi 2 baada ya kujifungua au zaidi kwa ushauri wa dk***
- ☑ ***Watoto chini ya miaka 18***
- ☑ ***Mfanyakazi yeyote mwenye uthibitisho wa daktari.***

**Mfanyakazi anayefanya Kazi za usiku anastahili Posho ya 5% (0.05) ya mshahara Wake wa saa.**

# MUDA WA MAPUMZIKO

- Mapumziko ya siku
- Mapumziko ya wiki
- Mapumziko ya wakati wa kazi

# Mapumziko ya siku

***(Kifungu No. 24 SAMK)***

*Mwajiri ni lazima ampe mfanyakazi mapumziko ya angalau saa 12 mfululizo kati ya muda anaomaliza kazi na muda atakaoanza kazi siku inayofuata.*

*Muda wa mapumziko unaweza kupungua hadi kufikia saa 8 kwa makubaliano ya maandishi pale ambapo mfanyakazi atapata mapumziko ya angalau saa 3 katikati ya saa za kazi za kawaida*

# Mapumziko ya wiki

***(Kifungu No. 24 SAMK)***

*Mwajiri ni lazima ampe mfanyakazi*
*angalau saa 24 mfululizo kati ya Siku ya kawaida ya mwisho ktk wiki*
*na ya kwanza ya kazi ya kawaida ya wiki inayofuata*

Mfanyakazi atayefanya kazi siku ya mapumziko kwa makubaliano na mwajiri ni lazima alipwe mara 2 ya mshahara wake wa saa kwa kila saa atakalofanya Kazi siku ya mapumziko

# Mapumziko ya wakati wa kazi
## *(Mapumziko ya chakula)*
***(Kifungu No. 23 SAMK)***

*Mwajiri ni lazima ampe mfanyakazi mapumziko*
*ya angalau dk 60 mfululizo*
*kwa ajili ya kupata chakula baada ya kufanya kazi*
*Kwa saa 5 mfululizo*

*Wakati wa mapumziko ya chakula mfanyakazi anaweza*
*Kuendelea na kazi iwapo kazi hiyo haiwezi kuachwa*
*Au kufanywa na mtu mwingine na*
*Anapaswa kulipwa*

# TARATIBU ZA MALIPO/ MISHAHARA (*Wages*)

***(Kifungu No. 27&28 SAMK)***

**RESPECT AND RIGHTS**

**Protection for domestic/household workers!**

**¡Protección para Trabajadoras Domésticas/Trabajadoras del Hogar!**

**Protection des travailleuses domestiques/employées de maison!**

Report of the international conference
held in Amsterdam, 8-10 November 2006

+
Highlights of post conference developments




**ILO CONVENTION 1919, No. 95**

***Protection of wages***

**SHERIA INAWATAKA WAAJIRI KUWALIPA MISHAHARA WAFANYAKAZI:**
***(Kifungu No. 27 SAMK)***



- ***Wakati wa saa za kazi***
- ***Mahali pa kazi***
- ***Katika siku iliyokubalika kuwa siku ya malipo***
- ***Kwa kuzingatia kipindi cha malipo i.e siku, wiki au mwezi kwa mujibu wa mkataba***
- ***Mwajiri ni lazima atoe 'salary slip'***

**◆Malipo yanaweza kufanyika kwa Fedha taslimu/hundi au kupitia Kwenye account ya mfanyakazi**

**◆Mfanyakazi anastahili kulipwa mshahara usiopungua kima cha chini cha mshahara Kilichopangwa kisheria**

# MAKATO (deductions)

*(Kifungu No. 28 SAMK)*

**Sheria inazuia waajiri kufanya makato ya aina Yoyote kutoka kwenye mshahara wa mfanyakazi Isipokuwa kama makato hayo yameruhusiwa**

**Mwajiri anaruhusiwa kukata makato yafuatayo toka kwenye Mshahara wa mfanyakazi:**

- ✓ **Kwa mujibu wa sheria, k.v kodi, michango ya penshen, Bima ya afya nk**
- ✓ **Kwa amri ya mahakama/tuzo ya mwamuzi *(arbitration award)***
- ✓ **Marejesho ya mkopo iwapo mfanyakazi ameridhia kwa maandishi**
- ✓ **Ada ya chama cha wafanyakazi baada ya kutoa idhini kwa fomu *(TUF.15)***

**Endapo mfanyakazi ataharibu mali za mwajiri kwa uzembe mwajiri anaweza kumkata mshahara wake kufidia Hasara iliyotokea.**

## Mwajiri anapaswa kuhakikisha kuwa:

- **Anazingatia utaratibu wa haki**
- **Hasara/uharibifu umetokea akiwa kazini na ni kosa la mfanyakazi**
- **Anampa mfanyakazi maelezo ya maandishi ya kiasi cha deni na chanzo cha uharibifu**
- **Mfanyakazi anapewa nafasi ya kujitetea na kupinga deni**
- **Jumla ya deni isizidi kiwango halisi cha hasara au uharibifu**
- **Makato yasizidi robo ya mshahara wa mfanyakazi**


# LIKIZO (Leave)

***(Kifungu 29 – 34 SAMK)***




**WAFANYAKAZI WAFUATAO WANASTAHILI LIKIZO YA MALIPO:**

- ☑ *Waliofanya kazi kwa zaidi ya miezi sita mfululizo*
- ☑ *Wafanyakazi wa msimu*
- ☑ *Waliofanya kazi kwa kipindi tofauti kwa mwajiri mmoja ktk mwaka iwapo vipindi husika vikijumlishwa vitazidi miezi sita.*



# LIKIZO YA MWAKA

*(Kifungu No. 31 SAMK)*

**Masharti ya likizo ya mwaka**

- *Mfanyakazi anastahili kupewa likizo ya siku 28 mfululizo ktk mzunguko wa miezi 12.*
- *Siku za likizo zinaweza kukatwa na mwajiri iwapo mfanyakazi alipewa ruhusa.*
- *Mwajiri anaweza kuamua siku ya kuanza likizo mfanyakazi ndani ya miezi sita kuanzia siku ambayo mfanyakazi alistahili kuanza likizo.*
- *Muda wa kuanza likizo baada ya miezi 6 unaweza kuongezwa kwa makubaliano iwapo yapo mahitaji ya uendeshaji na nyongeza ya muda wa kuanza likizo isizidi miezi 12.*
- *Mwajiri hatakiwi kumuomba mfanyakazi kufanya kazi katika muda wa likizo ya mwaka ya mfanyakazi.*
- *Hairuhisiwi kumlipa mfanyakazi pesa badala ya likizo – kununua likizo isipokuwa kwa makubaliano (Kanuni za 2017, 14 (2))*
- *Likizo ya mwaka haitakiwi kuchukuliwa wakati wa likizo nyingine.*
- *Mwajiri ni lazima amlipe mfanyakazi mshahara wake wakati wa likizo.*
- *Mwajiri ni lazima amlipe mfanyakazi malipo mengine yanayoambatana na likizo kwa mujibu wa Tamko au Amri ya kima cha chini cha mshahara na masharti ya ajira.*



# LIKIZO YA UZAZI KWA AKINA MAMA
**(Kifungu No. 33 SAMK)**




- *Mfanyakazi anastahili likizo ya uzazi ya malipo ya siku 84 au siku 100 iwapo atajifungua mtoto zaidi ya mmoja katika mzunguko wa miezi 36.*
- *Mfanyakazi analo jukumu la kutoa notisi ya ujauzito kwa mwajiri miezi 3 kabla ya tarehe anayotarajia kujifungua. ikiambatana na uthibitisho kutoka kwa Dr.*
- *Mfanyakazi anastahili kupewa saa mbili (2) kila siku kwa ajili ya kunyonyesha baada ya kumaliza likizo ya uzazi, kwa muda usiopungua miezi sita mfululizo*
- *Mwajiri anawajibika kutoa likizo ya malipo ya uzazi kwa vipindi vinne (4) tu.*
- *Mfanyakazi atastahili kupata likizo nyingine ya malipo ya siku 84 endapo mtoto amefariki ndani ya mwaka.*
- *Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009 zinaeleza kuwa kuwa endapo mtumishi ambaye hana sifa za kupewa likizo ya uzazi na pia hajafikia mzunguko wa likizo yake ya mwaka akajifungua, mwajiri atawajibika kumpatia likizo ya wiki 6 ambayo itakatwa katika likizo yake ya mwaka itakapofika. Kifungu H.12(5-6)*
- *Hata hivyo ni kinyume kumuachisha kazi mfanyakazi kwa sababu ya ujauzito au majukumu ya kifamilia.*



**LIKIZO YA UZAZI YA KINA BABA**

***(Kifungu No. 34 SAMK)***

- ***Mfanyakazi anastahili angalau siku 3 za likizo ya uzazi ya baba katika mzunguko wa miezi 36***
- ***Mfanyakazi atapoteza haki za likizo endapo atashindwa kuchukua likizo ndani ya siku 7 baada ya mtoto kuzaliwa***
- ***Mfanyakazi analojukumu la kuthibitisha kuwa mtoto aliyezaliwa ni wake***

# LIKIZO YA UGONJWA
## (Kifungu No. 32 SAMK)

- *Mfanyakazi anastahili likizo ya ugonjwa ya angalau siku 126 katika mzunguko wa miezi 36.*
- *Katika siku 63 za kwanza mfanyakazi anastahili malipo ya mshahara kamili.*
- *Katika siku 63 zinazofuata mtumishi anastahili malipo ya nusu mshahara.*
- *Kabla ya kuchukua likizo ya ugonjwa mfanyakazi anapaswa kuwasilisha kwa Mwajiri uthibitisho wa Daktari.*
- *Endapo mfanyakazi anastahili kulipwa wakati wa likizo ya ugonjwa kwa mujibu wa Sheria, mfuko wowote au makubaliano ya pamoja, Mwajiri atakuwa hana jukumu la kumlipa mfanyakazi huyo wakati wa likizo.*
- *Pale ambapo mtumishi atakuwa hajapona kwa kipindi hicho cha likizo ya ugonjwa mtumishi huyo anaweza kuachishwa kazi kwa sababu ya ugonjwa.*

# LIKIZO YA HURUMA
*(Kifungu No. 34 SAMK)*

**Mfanyakazi anastahili angalau siku nne (4) za likizo ya malipo katika mzunguko wa miezi 36 bila kujali idadi ya matukio kwa sababu zifuatazo:**

- **Kuugua au kifo cha mtoto.**
- **Kifo cha mke/mume, mzazi, babu, bibi, mjukuu au ndugu wa kuzaliwa.**

> ***Kwa mujibu wa kanuni za utumishi, Mfanyakazi anastahili angalau siku 14 za likizo bila kujali idadi ya matukio kwa sababu mbalimbali kama:kuugua au kifo cha mtoto,kifo cha mke/mume/mzazi.***

# Likizo ya viongozi wa vyama vya wafanyakazi

- **Viongozi wa vyama vya wafanyakazi wana haki ya kupewa likizo kwa ajili ya kuhudhuria katika vikao, mikutano ya vyama vya wafanyakazi**
- Mtumishi atahesabika kama anatekeleza majukumu yake ya kazi pale ambapo atakuwa amehudhuria katika mikutano ya vyama vya wafanyakazi na mwajiri atalazimika kugharamia gharama zote za safari ya mfanyakazi.
- *KANUNI ZA KUDUMU UTUMISHI WA UMMA 2009, H.14(2)*

# Safari za kikazi

- **Safari za kikazi ni moja ya mambo yanayojitokeza kwa mtumishi katika kutekeleza majukumu yake ya ndani na nje ya nchi.**
- **Serikali italazimika kumlipia usafiri mtumishi kwa safari za kikazi endapo mfanyakazi atakuwa:**
  - Anatekeleza majukumu yake.
  - Kuhamishwa
  - Likizo
  - Kusitishwa kwa ajira
  - Kupatiwa matibabu ya ziada
  - Kuhudhuria semina, mikutano au mafunzo yaliyothibitishwa na mwajiri.
  - Ajira ya kwanza.
- **Hata hivyo malipo ya usafiri katika uhamisho ni lazima yafanyike kabla ya mtumishi kuripoti katika kituo kipya cha kazi**


# LIKIZO YA KUSTAAFU

- Mtumishi atastahili kuomba likizo ya kujiandaa kustaafu ndani ya miezi sita kabla ya tarehe rasmi ya kustaafu kwake.
- Wakati wa kustaafu kwa mtumishi, Mwajiri Atastahili kugharamia posho ya kujikimu na nauli

# Hitimisho

**Muda wa likizo unaweza kuongezwa kutokana na maboresho ya Mkataba wa Hali Bora (Collective Bargaining Agreements-CBA)**







Profit
Sale
Family
Hardwork
boss
Hobbies
Refreshing
Management
Presentation
Kids
Quality Time
Meeting
Visit
Happiness
Relax
Overtime
love
Work-Life Balance



# What Keeps Employees Happy?

A survey of workers in 1999 revealed the key elements that lead to employee satisfaction.



# Q & A

**THANK YOU FOR LISTENING AND SHARING!**

